Mitazamo Mitano Ya Marko 16:16

na

Ellis P. Forsman

Mitazamo Mitano Ya Marko 16:16

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Mitazamo Mitano Ya Marko 16:16

Jinsi Baadhi ya watu watakubali uwazi

Kuna tamko la Yesu ambalo liko wazi, nab ado inachanganya, ambapomara chache unasikia ikitumiwa na wahubiri wa madhehebu, ama katika makanisa yao au kwenye runinga au redioni. Kwamba wanapofanya, wanajisikia kama ni muhimu kutoa maelezo ambayo yankwenda kinyume na kauli ya Yesu.

Nimetumia maneno ambayo Yesu aliongea katika: Marko 16:16, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."*

Kuonyesha kile nilichosema, hebu na tuangalie mitazamo tofauti minne ya misitari hii kama inavyofundishwa na wanadamu, na ulinganishe mitazamo hiyo na ile ya wazi ambayo Yesu alitoa na ikaungwa mkono na mitume wake katika kufundisha na kuhubiri kwao.

Mtazamo wa kwanza ni ule unaoshikiliwa na wale ambao hawafikirii kuwa Wakristo, lakini kwa kusudi la somo letu itazingatiwa.

Kwa mtazamo watasema…

Aaminiye na kubatizwa "hata" okoka

Makundi mawili tofauti wanashikilia mtazamo huu:

- MAPAGANI – Wale wasio mwamini Mungu, mbingu au motoni, au wokovu wa namna yoyote.
- WAYAHUDI, WAISILAMU, WAHINDI, nk., wanaoamini Mungu (au miungu), lakini hawaamini kwamba wokovu unapatikana kwa Yesu, na ya kwamba kuamini na/ au ubatizwe ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Lakini wale wanao mkubali Yesu na mamlaka ya mitume wake wanakataa mtazamo huo.

Kuna Mungu anayetoa wokovu (kinyume na mtazamo wa asiyemwamini Mungu). 1 Tim. 2:3-4, *"Hili ni zuri nalo lakubalika mbele za Mungu mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliokweli."*

Wokovu UNA kujakupitia Yesu (kinyume na Wayahudi, Waisilamu, Wahindi, nk).

- 1 Tim. 2:5-6, *"Kwa sababu Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Yesu Kristo."*

- Yoh. 14:6, *"Yesu akamwambia mimi ndimi njia na kweli, na uzima mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."*

Kuna baadhi katika dunia wanaoamini hili, na inaanza kueleza jinsi baadhi wanapenda kukataa kauli ya wazi ya Yesu. Hakika, wale wanaoshikilia mtazamo huu hawawezi kusoma Agano Jipya.

Zingatia mtazamo wa pili...

Yeye "asiyeamini" na "asibatizwe" ataokolewa

Hii inashikiliwa na "ulimwengu mzima" wanaoamini kwamba Mungu ataokoa kila mmoja maramoja.

Kuunga mkono mtazamo wao, watatupilia mbali misitari kama 1 Tim. 2:6, *"Ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote utakaoshuhudiwa kwa majira yake."*

Lakini wale wanaojua *mafundisho ya Kristo wanakataa mtazamo huo. Yesu mwenyewe alisema kwamba kutakuwa na wachache watakaokolewa.*

Math. 7:13-14, *"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani nao walionao ni wachache."*

Paulo alionya wale ambao wasinge okolewa, lakini wangekutana na hasira ya Mungu. Waef. 5:5-6, *"Maana neno hili mnalijua hakika yakwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tama, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu. Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu huwajia wana wa uasi."*

Wengi "Wanaoamini Biblia, wanatabiri Wakristo" hawata chukuliana na Mark 16:16 jinsi mitazamo miwili ya kwanza ilivyo. Lakini tunapoangalia mitazamo miwili zaidi, tunaweza kuanza kugusa "nyumbani".

Lakini tafadhali elewa, kwamba tunafanya hivyo, tukitamani "kuongea ukweli kwa upendo"; na tunaomba kwamba upendo wenu kuhusu ukweli ni ule ambao mnatamani kuzingatia kinachofuata:

Matend. 17:11, *"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku waone kwamab mambo hayo ndivyo yalivyo."*

Mtazamo wa tatu...

“Asiyeamini” na “kubatizwa” ataokolewa

Mtazamo huu unashikiliwa na wale wanao “wabatiza vichanga”.

Kwa “kubatiza” (kunyunyiza, si kuzamishwa) watoto wachanga ambao hawajui maana ya imani, wana (zaidi sana Wakatholiki) wanaonyesha kwamba imani si muhimu katika wokovu. Wengine (sanasana Walutheri) wanajaribu kuwa karibu na hili kwa kusema kwamba Mungu kwa sehemu imani inayookoa kwa vichanga (watoto) kwa hiyo ubatizo bado unaweza kuokoa.

Kwaku nyunyiza au kumwagiliza badala ya kuzamishwa, pia wanaonyesha kwamba Yesu hakumaanisha kile alichokisema (sababu “BATIZWA” hapo juu iko katika nukuu)

Lakini kuongea ukweli kwa upendo.....

Imani hiyo ni muhimu kwa hatua.

Kwa ubatizo – Matend. 8:35-37*, “Filipo akafunua kinywa chake naye akianza na andiko lilo hilo akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji Yule Towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo <u>akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana</u>, akjibu akasema naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu.”*

Kwa wokovu – Waru. 10:9-10*, “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana <u>na kuamini moyoni mwako</u> ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri **hatakupata** wokovu.”*

Ni ubatizo pekee ndiyo umweka mtu **<u>KATIKA</u>** Kristo.

Lazima pia tuonyeshe kwamba kunyunyiza au kumwaga SIYO ubatizo wa kibiblia.

Neno la Kiyunani lililotumika katika Biblia ni “baptizmo”, na inamaanisha “kuzamisha”.

Hii ndiyo maana ubatizo unaelezwa katika Biblia kuwa ni “maziko”.

- Waru. 6:3-4*, “Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulizikwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.”*

- Wakol. 2:12, *"Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo na katika huo mkafufuliwa pamoja naye kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu."*

Miji yenye misiba huwa wana weka udongo kidogo juu ya marehemu?

Kunyunyiza au kumimina iliondolewa ikawekwa ubatizo (Kuzamishwa) miaka mamia baada ya Kristo na mitume wake. Hii ikawa ni desturi katika ulimwengu wa kidini.

Kwa kutunza "*desturi za wanadamu"* kwa kunyunyiza au kumimina, tunashindwa kutunza "*Amri ya Mungu"* kuhusu ubatizo. Yesu anakataa kuondoa neno la Mungu na kuweka maagizo ya wanadamu.

Math. 15:3-9, *"Akajibu akawambia mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu? Kwa kuwa Mungu alisema, mheshimu baba yako na mama yako na amtukanaye baba yake au mama yake kufa na afe. Bali ninyi husema atakayemwambia babaye au mamaye, chochote kikupasacho kusaidiwa na mimi ni wakfu, basi asimuheshimu babaye au mamaye. Mkalitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu. Enyi wanafiki ni vyema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu akisema, watu hawa uniheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali name. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu."*

Lazima pia tuonyeshe kuwa kuwabatiza watoto wachanga haipokimaandiko. Hakuna amri au mfano wa vichanga kubatizwa katika Biblia.

Kwa sababu mizizi ya imani (Marko 16:16; Matend 8:37) na toba (Matend. 2:38) ziko juu ya uwezo wa watoto, hivyo si watahiniwa wa ubatizo.

- Marko 16:16, *"<u>Aaminiye</u> na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."*
- Matend.8:37, *"Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana, akajibu akasema <u>naamini ya kuwa Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu."</u>*
- Matend. 2:38, *"Petro akawambia <u>tubuni mkabatizwe</u> kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*
- Matend. 17:30, *"Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa <u>anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu."</u>*

Nina ujasiri kwamba hao wanao shikilia mtazamo wa kunyunyizia vitoto vichanga ni wa kweli na hawana hatia. Lakini bila kujali ukweli

wao, bado wanahatia ya kubadilisha maneno ya Yesu kama hao wasiyo muamini Mungu, Wayahudi wasioamini (na Waisilamu, Wahindi, nk.) na ulimwengu mzima.

Lakini kuna mtazamo mwingine ukweli unaoshikiliwa na wengi, na hiyo ni.....

Aaminiye na "hasi" batizwe ataokoka

Mtazamo huu unashikiliwa na wale wanaoamini wokovu kwa imani "pekee"; kwamba mtu anaokolewa KABLA ya ubatizo; kwamba ubatizo si muhimu kwa wokovu.

Mtazamo huu unashikiliwa kwa ajili ya matendo ya kinadharia na washiriki wengi wa madhehebu. Lakini Yesu na mitume wake kwa uwazi walifundisha tofauti.

Kwamba imani "pekee" haiwezi kuokoa.

Kama ilivyosemwa na Yesu.

- Math. 7:21, *"Si kila mtu aniambiaye Bwana Bwana ataingia katika ufalme wa mbinguni, bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu wa mbinguni."*
- Luka. 6:46, *"Na kwa nini mnaniita Bwana Bwana, walakini hamyatendi nisemayo."*

Kama ilivyofundishwa na mitume wake.

- Waru. 6:17-18, *"Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa miyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki."*
- Waeb. 5:9, *"Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii."*
- Yakob. 2:14, *"Ndugu zangu yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani yaweza kumwokoa"?*
- Yakob. 2:17, *"Vivyo hivyo na imani isipokuwa inamatendo, imekufa nafsini mwake."*
- Yakob. 2:20, *"Lakini watakakuju wewe mwanadamu usiye kitu, kwa imani pasipo matendo haizai"?.*
- Yakob. 2:24, *"Mwaona kuwa mwanadamu uhesabiwa kuwa anahaki kwa matendo yake, si kwa imani peke yake."*

- Yakob. 2:26, *"Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa."*
- 1 Yoh. 2:3-4, *"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, nimemjua wala hazishiki amri zake ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake."*

Maandiko yanafundisha kuwa ubatizo **ni** muhimu kwa wokovu.

Kulingana na Yesu.

- Yoh. 3:5, *"Yesu akajibu, Amin amin nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuingia ufalme wa Mungu."*
- Marko 16:16, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."*
- Math. 28:18-20, *"Yesu akaja kwao akasema nao akwambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*

Kulingana na mitume wake.

- Matend. 2:38, *"Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*
- Anania alimwambia Paulo katika Matendo 22:16, *"Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake."*
- Wagal. 3:26-27, *"Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo."*
- Wakol. 2:12-13, *"Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo, na katika huo mkafufuliwa pamoja naye kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu. Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu aliyafanya hai pamoja naye akiisha kutu samehe makosa yote."*
- Tito 3:5, *"Si kwa matendo ya haki tuliyoyatenda sisi bali kwa rehema yake kwa kuoshwa, kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu."*

- 1 Petr. 3:21, *"Wapenzi mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu."*

Tena, nina amini kwamba wale wanaoshikilia mtazamo huu (ukiunganisha ndugu binafsi) ni wa kweli, na hawajui kwamba wana badilisha maneno ya Yesu. Alafu, siwezi kusaidia bali kufikiria kuhusu watu hawa kama jinsi Paulo alivyo wafikiria ndugu zake wa kimwili.

Waru. 10:1-3, *"Ndugu zangu nitakayo sana moyoni mwangu na dua yangu nimwombayo Mungu ni kwa ajili yao ili waokolewe. Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa. Kwa maana wakiwa hawajui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.*

Hii inatuongoza katika hatua ya tano na mwisho wa mtazamo, moja ambayo naamini kuna msukumo wa kuikubali.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka

Mtzamo huu unachukua maneno ya Yesu katika thamani ya hali ya juu. Hakuna maelezo ambayo ni ya muhimu. Yesu anasema kile anachoamini, na anamanisha kile anachokisema.

Tayari tumeshaona hapo nyuma kwamba Biblia inafundisha.....

Kwamba mtu lazima "aamini".

Matendo. 8:36-37, *"Wakawa wakiendelea njianiwakafika mahali penye maji, yule Towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame wakatelemka wote wawili majini Filipo na Yule towashi naye akambatiza."*

Kwamba mtu lazima "abatizwe" ili kufurahia msamaha wa dhambi.

Matend. 2:38, *"Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi matapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Mwisho

Ni yapi kati ya mitazamo mitano ya Marko 16:16 unapenda kuwa nayo?

- Aaminiye na kubatizwa “hata” okoka?
- “Asiyeamini” na “asiyebatizwa” ataokoka?
- “Asiyeamini” na “kubatizwa” ataokoka?
- Aaminiye na “asibatizwe” ataokoka?
- Aamniye na kubatizwa ataokoka?

Na iwe wazi kwamba kuna mtazamo mmoja tu ambao unaendana na maneno ya Yesu, kama jinsi kuna moja ambayo haihusu “kupindua” kauli ya wazi ya Yesu.

Lakini labda mhimu zaidi, ni yapi katika mitazamo hii mitano ambayo maisha yako yanaendana?

Mtu anaweza kuchagua nambari ya TANO, lakini akajifanya kwamba anachagua mtazamo wa PILI.

Kivipi? Kwa kutokiri imani katika Kristo na kubatizwa!

Mtu anaweza kushikilia nambari ya TANO, lakini wakajifanya kwamba wanaamini mtazamo wa TATU.

Kivipi? Hatakama watakuwa wame “batizwa”, hawaishi maisha ya imani inayotakiwa na Yesu!

Mwingine anaweza kushikilia mtazamo wa TANO, lakini wakajifanya wanaamini mtazamo wa NNE.

Kivipi? Kwa maana wakati wanamwamini Yesu Kristo, hawajajitoa ili kubatizwa!

Ni wale tu waliokuja kwa Yesu kwa imani na WAKAENDANA na mafundisho yake, anaweza akawa na uhakika wa wokovu. Maneno ya Biblia yapowazi.

- Matend. 2:38, *“Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”*
- Matend. 22:16, *“Basi sasa unakawilia nini? Simam ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.”*